**Kaunti ya King • Ofisi ya Usimamizi ya Utekelezaji wa Sheria (OLEO)**

# MFUMO WA MWONGOZO WA JAMII KWA UKAGUZI WA SERA

King County OLEO

Hati hii inatoa muhtasari wa mchakato wa mwongozo wa jamii ya OLEO kwa ukaguzi wa sera. Kulingana na sheria, OLEO ina mamlaka ya kukagua na kutoa mapendekezo kwa Liwali kuhusu mabadiliko katika sera, kanuni, taratibu, au maagizo ya jumla ya Ofisi ya Liwali (Sheriff's Office) [Kanuni za Kaunti ya King (King County Code, K.C.C.) 2.75.040(D)]. Pamoja na programu zake zingine,

**OLEO inalenga kuboresha viwango vya utekelezaji wa sheria kupitia mapendekezo ya sera yanayotokana na ushahidi, unaoongozwa na jamii, na yaliyojikita katika usawa.**

Kwa kushughulikia lengo hilo, OLEO imeunda mchakato wa kukagua na kuendeleza mapendekezo ya sera kwa kushirikiana na kushauriana moja kwa moja na jamii. Mwongozo huu unazidi kupigwa msasa, na tunawaalika wakazi wa Kaunti ya King kuwasiliana nasi ikiwa wangependa kushiriki au kutoa maoni yao.

## MKAKATI

1. **Tambua Hitaji la Mabadiliko ya Sera** →
2. **Ukaguzi wa Awali wa Sera** →
3. **Kuamua Kiwango cha Mwongozo wa Jamii** →
4. **Kuandaa Rasimu ya Sera** →
5. **Kusimamia Utekelezaji, Kuelezea Athari ya OLEO, na Kutathmini Mchakato** →
6. **Elimu ya Jamii**

**Kwa maelezo zaidi**, tembelea **tovuti ya OLEO** au tuma barua pepe kwa **OLEO@kingcounty.gov**.

## 1 Kutambua Hitaji la Mabadiliko ya Sera

**Ukaguzi wa sera unaweza kuanzishwa kupitia:**

- Uamuzi wa Ofisi ya Liwali ya Kaunti ya King
- **Mwongozo wa Kamati ya Ushauri ya Wananchi kuhusu Usimamizi wa Utekelezaji wa Sheria (Community Advisory Committee for Law Enforcement Oversight, CACLEO)**
- Shauku kubwa ya jamii
- Mabadiliko ya sheria au maamuzi ya mahakama
- Matokeo ya Uchunguzi wa OLEO
- **Utafiti wa Mpango wa Sera wa OLEO**
- **Jitihada za Kushirikisha Jamii kupitia OLEO**

***Je, sera hii inapaswa kupewa kipaumbele kwa ukaguzi?***

Iwapo **yoyote** kati ya haya yamejibiwa ndiyo, endelea. Ikiwa tatu zimejibiwa "hapana," ukaguzi wa sera hii hautapewa kipaumbele.

- *Je, sera hii au mabadiliko ya sera yanaathiri jamii ambazo zimeathirika au zilizoathirika sana na utekelezaji wa sheria?*
- *Je, sera inasimamia mwingiliano wa moja kwa moja au unaoendelea kati ya wanajamii na wafanyakazi wa Ofisi ya Liwali?*
- *Je, sera hii inahusisha masuala ya maisha na usalama wa wanajamii?*

## 2 Ukaguzi wa Awali wa Sera

**OLEO hufanya ukaguzi wa awali ya kila sera inapofaa.**

1. UKAGUZI WA SERA
Chambua lugha, ufafanuzi, na istilahi kuhakikisha lugha iko wazi na haiwezi kufasiriwa visivyo.

2. UKAGUZI WA MASHIRIKA SAWIA
Linganisha na mashirika mengine ya utekelezaji wa sheria.

3. UKAGUZI WA TARATIBU BORA
Fanya utafiti na kurejelea mashirika kama Muungano wa Uhuru wa Kiraia wa Marekani(American Civil Liberties Union, ACLU), Chama cha Kimataifa cha Wakuu wa Polisi(International Association of Chiefs of Police, IACP), nk.

4. KAGUA RIPOTI ZA AWALIZA *OLEO* NA ZA OFISI YA MKAGUZI WA KAUNTI YA KING (KING COUNTY AUDITOR'S OFFICE, *KCAO).*
Pitia mapendekezo ya awali kuhakikisha mabadiliko yanalingana.

5. TATHMINI UHALISIA
Tathmini utekelezaji katika sekta husika na kwa kuzingatia hali ya kijamii na maoni ya umma.

## 3 Amua Kiwango cha Mwongozo wa Jamii

**MRADI WA SERA UNAOONGOZWA NA JAMII:**
Mchakato wa ushirikiano na jamii na OLEO kuunda sera.

***AU***

**UKAGUZI WA HARAKA (RAPID-RESPONSE REVIEW):**
Mchakato wa Ushauri: OLEO huunda bidhaa ya sera na kuituma kwa jamii kwa maoni.

***Je, kuna haja ya dharura kwa mabadiliko ya sera?***

Ikiwa jibu ni ndio, endelea hadi **Hatua ya 4** na Ukaguzi wa Haraka. Ikiwa hapana, jibu maswali yafuatayo. Kujibu yoyote ya maswali haya "ndiyo" kutaelekeza Mradi wa Sera Unaoongozwa na Jamii katika Hatua ya 4.

- ***Je, wanajamii wana ujuzi na uwezo unaohitajika katika kutoa maoni faafu?***
- ***Je, pendekezo la sera linatofautiana kwa kiasi kikubwa na mazoea ya sasa ya Ofisi ya Liwali (mfano, uandikaji mpya kabisa dhidi ya marekebisho madogo)?***
- ***Je, suala hili la sera linaangazia mahitaji ya wanajamii?***

*Iwapo una shaka, tafuta* ***maoni kutoka kwa Mashirika ya Mashaurianoya*** *Jamii.*

## 4 Rasimu ya Sera

**MRADI WA SERA UNAOONGOZWA NA JAMII**

- Tambua washikadau.
- Kuunda ***Jopo Kazi la Washikadau***. Miradi hii inakusudiwa kuwa ya muda mrefu na inaweza kudumu miezi 6-12 kutegemea na wigo wa mradi.
- ***Jopo Kazi la Washikadau*** linaweza kubaini kuwa ni muhimu/inafaa kupeleka mapendekezo ya haraka kwa ***Ofisi ya Liwali***.
- Jamii na OLEO hushirikiana kubuni sera/mapendekezo/ripoti ya utafiti.
  - Eleza tatizo, jadili chaguo za sera na mbadala.
  - Amua maadili na malengo.
  - Fikia makubaliano – elewa athari inayowezekana, jadili upatikanaji, usawa, na uchaguzi wa lugha jumuishi.
- Kushauriana na ***Jopo Kazi la Washikadau*** ili kuamua haja ya ushirikiano zaidi.
- Kamilisha sera (barua, ripoti ya utafiti, lugha ya sera, nk.).
- Tuma kwa ***Ofisi ya Liwali***.

***Jukumu la OLEO: Kushirikiana***

***AU***

**UKAGUZI WA HARAKA**

- OLEO inatayarisha muhtasari wa awali wa mapendekezo kulingana na **Hatua ya 2: Ukaguzi wa Awali wa Sera**.
- Shiriki na ***Mashirika ya Mashauriano ya Jamii*** kwa muda wa wiki mbili.
- Jumuisha maoni kutoka kwa mashirika ya mashauriano.
- Tuma mapendekezo ya mwisho kwa ***Ofisi ya Liwali***.

***Jukumu la OLEO: Kushauri***

## 5 Kuelezea Athari na Kutathmini Mchakato

- Chapisha mapendekezo ya sera kwenye tovuti ya OLEO na ujulishe ***Mashirika ya Mashauriano ya Kijamii (Community Consulting Organizations)*** au ***Jopo la Washikadau kuhusu*** hatua inayohitajika, ikiwa ipo.
- Fuatilia utekelezaji wa sera ***ya Ofisi ya Liwali*** na majibu ya jamii.
- Shiriki taarifa kupitia jarida, kifuatiliaji sera, ripoti ya kila mwaka, nk.
- Kusanya maoni kuhusu mchakato.

! *Tathmini kila mwaka ili kuboresha mchakato wa ukaguzi wa sera na kuhakikisha maslahi ya jamii yanazingatiwa*

## 6 Elimu ya Jamii

- Andaa nyaraka za kuelezea au video za kielimu kuelezea umuhimu wa suala la sera.
- Jiunge na mikutano ya jamii na andaa warsha kushiriki mipango ya sera ya OLEO.
- Andaa mafunzo ya kuimarisha uwezo kwa wanaoathiriwa zaidi na sera.
- Unda maktaba ya rasilimali za programu na vifaa vya nje vinavyohusiana.
- Shirikiana na mashirika ya jamii kukuza rasilimali kwa mahitaji ya kielimu na kibinafsi.

***Jukumu la OLEO: Kuelimisha***